

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA**  
**(Barua zote zipelekwe Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa)**

Simu: 2525 – 0255 25-2802163  
Nukushi: 0255 25-2802163  
Baruapepe:  
[md@sumbawangamc.go.tz](mailto:md@sumbawangamc.go.tz)  
Tovuti. [www.sumbawangamc.go.tz](http://www.sumbawangamc.go.tz)



Mkurugenzi wa Manispaa ,  
S.L.P. 187,  
**SUMBAWANGA**

**10 Januari 2023**

**TAARIFA KWA UMMA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga inawatangazia na kuwakumbusha wafanyabiashara wote;

- ❖ Kuhuisha leseni za biashara zilizokwisha muda wa matumizi.
- ❖ Kulipia ushuru wa huduma (Service Levy)

Malipo yote ya **Leseni za Biashara** na **Ushuru wa Huduma** (Service Levy) yafanyike katika Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa chumba namba 13 ( Ofisi ya Biashara)

Aidha kila mfanyabiashara anatakiwa kuhakikisha kuwa ana leseni ya biashara kwenye biashara yake.

Ukaguzi wa **Leseni za Biashara** na **Ushuru wa Huduma** utafanyika kuanzia tarehe 16 Januari 2023 katika maeneo yote ya Manispaa ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Biashara Na. 25 ya mwaka 1972

Hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya yeyote ambaye atabainika kufanya biashara bila kuhuisha leseni, kufanya biashara bila kuwa na leseni au kufanya biashara bila kulipa ushuru wa huduma. Pamoja na hatua nyinginezo atakayebainika kukiuka Sheria ya Biashara atalipa faini isiyopungua Tsh 200,000/=

Imetolewa na

Khadija Dalasia  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Manispaa ya Sumbawanga

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA  
(Barua zote zipelekwe Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa)**

Simu: 2525 – 0255 25-2802163  
Nukushi: 0255 25-2802163  
Baruapepe:  
[md@sumbawangamc.go.tz](mailto:md@sumbawangamc.go.tz)  
Tovuti. [www.sumbawangamc.go.tz](http://www.sumbawangamc.go.tz)



Mkurugenzi wa Manispaa ,  
S.L.P. 187,  
**SUMBAWANGA**

**10 Januari 2023**

**TAARIFA KWA UMMA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga inawatangazia wananchi wote kuwa kwa mujibu wa Sheria za Mipango Miji ni marufuku kufanya ujenzi na maendeleo ya aina yoyote ndani ya eneo la Manispaa bila ya kuwa na kibali cha Ujenzi.

Wananchi wote ambao wanaendelea na ujenzi katika maeneo mbalimbali ndani ya eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga wanaelekezwa kuhakikisha wanalipia kibali cha ujenzi kabla ya kuanza shughuli yoyote ya ujenzi katika maeneo yao.

Kibali cha ujenzi kinatolewa kwa gharama ya Tsh 40,000/= kwa ujenzi wa majengo ya makazi. Kinatolewa kwa gharama ya Tsh 100,000/= kwa ujenzi wa majengo ya makazi-biashara, na Tsh 200,000/= kwa majengo ya biashara.

Malipo yote ya vibali vya ujenzi yafanyike katika Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa chumba namba 5 ( Ofisi ya Malipo) au katika Ofisi ya Mtendaji wa Kata ambako ujenzi husika unakusudiwa kufanyika.

Kumbuka kuwa kibali cha ujenzi kinakatwa kabla ya ujenzi husika kuanza, ikibainika ujenzi ulianza kabla ya kibali kutolewa mhusika atawajibika kulipa kibali cha ujenzi pamoja faini kwa mujibu wa Sheria.

Ukaguzi wa vibali vya ujenzi kwa maeneo yote ambayo ujenzi unaendelea utafanyika kuanzia tarehe 16 Januari 2023.

Imetolewa na

Khadija Dalasia  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Manispaa ya Sumbawanga

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA  
(Barua zote zipelekwe Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa)**

Simu: 2525 – 0255 25-2802163  
Nukushi: 0255 25-2802163  
Baruapepe:  
[md@sumbawangamc.go.tz](mailto:md@sumbawangamc.go.tz)  
Tovuti. [www.sumbawangamc.go.tz](http://www.sumbawangamc.go.tz)



Mkurugenzi wa Manispaa ,  
S.L.P. 187,  
**SUMBAWANGA**

**10 Januari 2023**

**TAARIFA KWA UMMA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga inawatangazia na kuwakumbusha wamiliki wote wa malori kuhakikisha yanaegeshwa katika maeneo rasmi ya yaliyotengwa kawa ajili ya maegesho. Kituo cha maegesho ya malori kiko Utengule.

Gharama za kugesha lori katika Kituo cha Maegesho cha Utengule ni tsh 5,000/= kwa siku. Malipo ya gharama za maegesho yatafanyika katika kituo cha maegesho.

Aidha wamiliki wote wa magari madogo wanawajibika kulipia ushuru wa maegesho kiasi cha Tsh 1,000/= kwa siku kwa maeneo yote ndani ya Manispaa ya Sumbawanga.

Kuanzia tarehe 16 Januari 2023 litafanyika zoezi maalum la ukaguzi, ambalo litakuwa endelevu katika maeneo yote ya Manispaa ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Maegesho

Yeyote ambaye atabainika kugesha gari katika maeneo ambayo siyo rasmi au atashindwa kulipa ushuru wa maegesho hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni Pamoja na kulipa faini isiyopungua Tsh 200,000/=

Wamiliki wa malori na magari madogo wanasisitizwa kuhakikisha wamepatiwa risiti ya kieletroniki ambazo zinaweza kuhitajika wakati wowote kwa ajili ya uhakiki na ukaguzi.

Imetolewa na

Khadija Dalasia  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Manispaa ya Sumbawanga

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA  
(Barua zote zipelekwe Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa)**

Simu: 2525 – 0255 25-2802163  
Nukushi: 0255 25-2802163  
Baruapepe:  
[md@sumbawangamc.go.tz](mailto:md@sumbawangamc.go.tz)  
Tovuti. [www.sumbawangamc.go.tz](http://www.sumbawangamc.go.tz)



Mkurugenzi wa Manispaa ,  
S.L.P. 187,  
**SUMBAWANGA**

**10 Januari 2023**

**TAARIFA KWA UMMA**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga inawatangazia wamiliki wote wa nyumba za kulala wageni kuhakikisha kuwa wageni wote wanaolala katika nyumba za kulala wageni wanasajiliwa katika kitabu cha wageni kilicho rasmi kinachotolewa na Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa.

Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anatakiwa kuwasilisha kitabu kwa ajili ukaguzi, kufanyiwa mahesabu na kulipa ushuru wa hoteli kila tarehe 25 hadi tarehe 30 ya kila Mwezi.

Malipo yote ya ushuru wa hoteli (hotel levy) yafanyike katika Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa **Chumba Namba 13** (Ofisi ya Biashara) kwa wamiliki wa nyumba zote za kulala wageni ambao hawasajiliwa kulipa kulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT)

Aidha kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anatakiwa kuwa na leseni ya biashara iliyo hai na vyeti vya afya kwa watumishi wake vilivyo hai, kwenye biashara yake.

Zoezi la ukaguzi katika nyumba za kulala wageni litafanyika kuanzia tarehe 16 Januari 2023 katika maeneo yote ya Manispaa ikiwa ni utekelezaji wa kifungu cha 26 (2) Sheria Na. 105 ya Mwaka 1965 pamoja na marekebisho yake.

Yeyote ambaye atabainika hajalipa ushuru wa hoteli (hotel levy), bila kuwa leseni ya biashara iliyo hai bila kuwa na vyeti vya afya kwa watumishi wake Pamoja na ukiukaji mwingine wowote wa Sheria hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kulipa faini isiyopungua Tsh 200,000/=

Imetolewa na

Khadija Dalasia  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Manispaa ya Sumbawanga

